

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Simu ya Upepo “**SEKRETARIETI**”
Simu: 255 (026) 2963652
Tovuti: www.ajira.go.tz
Barua:Pepe:katibu@ajira.go.tz



Sekretarieti ya Ajira katika
Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM) na
Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro,
S. L. P. 2320,
DODOMA.

Dodoma
26 Januari, 2025

TAARIFA KWA UMMA

**USAILI WA WALIMU DARAJA LA IIIC - KISWAHILI KUFANYIKA TAREHE 30 JANUARI,
2025 BADALA YA 28 JANUARI, 2025**

Katibu, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anapenda kuujulisha umma kuwa usaili wa Walimu Daraja la IIIC – Kiswahili uliopangwa kufanyika tarehe 28 Januari, 2025 katika vituo mbalimbali nchini, sasa utafanyika tarehe 30 Januari, 2025 kuanzia saa 1.00 Asubuhi.

Mabadiliko haya yametokana na uwepo wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati utakaofanyika Jijini Dar es Salaam, uliosababisha kufungwa kwa baadhi ya barabara tarehe 27 na 28 Januari, 2025. Hali hii inaweza kusababisha changamoto ya usafiri kwa wasailiwa wanaotoka katika Jiji hilo na hivyo kushindwa kufika katika vituo vyao vya usaili kwa wakati.

Tarehe nyingine za usaili, mahali pa kufanyia usaili na muda wa usaili utabaki kama ulivyo kwenye matangazo ya awali ya kuitwa kwenye usaili.

Lynn D. Chawala
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini